**TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA TUWASA ENG. MAYUNGA ANTHONY KASHILIMU KUHUSU MRADI WA UJENZI WA MABWAWA YA KUTIBU MAJITAKA YANAYOKUSANYWA KWA NJIA YA MABOZA KATIKA MANISPAA YA TABORA.**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dr. Batilda Salha Burian na Viongozi wote wa Serikali mliopo hapa**

**Mhe. Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tabora, Mzee Hassan Wakasuvi (Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi) pamoja na viongozi wote wa Chama mliopo**

**Ndugu Dick Mlimuka, Mwenyekiti wa Bodi ya TUWASA pamoja na Wajumbe wa Bodi mliopo**

**Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa**

**Wahandisi kutoka Wizara ya Maji**

**Ndugu Viongozi wa Taasisi za Serikali mliopo**

**Menejimenti ya TUWASA,**

**Waandishi wa Habari,**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania………………**…..

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Kwanza kabisa, kwa niaba ya Bodi ya TUWASA, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wetu wa kuja kuwa mgeni rasmi katika hafla hii ya utiaji saini mradi wa ujenzi wa mabwawa ya Majitaka yanayokusanywa kwa njia ya magari/maboza. Sisi sote tunafahamu jinsi ulivyo na majukumu mengi ya Kimkoa lakini umetupa heshima hii, tunashukuru sana.

Aidha, natoa shukurani kwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wetu wa Tabora, Mzee Hassan Wakasuvi kwa kukubali kutenga muda wake adhimu kuja kuungana na wewe katika hafla hii. Yeye ndiye mwenye duka na sisi ni wauzaji wa duka hilo. Tunajisikia faraja sana kumwona mwenye mali ameungana nasi leo kushuhudia utekelezaji wa Ilani ya Chama kinachosimamia serikali.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Tabora kwa sasa ni wastani wa asilimia 94. Hii imetokana na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali pamoja na Chama tawala (Chama cha Mapinduzi) ya kutekeleza mradi mkubwa ya maji kutoka ziwa Viktoria kupitia Miji ya Shinyanga, Igunga, Nzega, Isikizya hadi Manispaa ya Tabora. Zaidi ya shilingi Bilioni 640 zilitumika kutekeleza mradi huo mkubwa ambao ulikamilika mwezi Februari mwaka 2020. Maji yanayozalishwa kwa sasa katika Manispaa ya Tabora ni Wastani wa lita 19,500,000 kwa siku.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Ongezeko hili la majisafi pia linapelekea ongezeko la uzalishaji wa majitaka hasa ukizingatia ukweli kuwa asilimia 80 ya majisafi yanayotumika katika familia hugeuka kuwa Majitaka (*Wastewater*). Hivyo, uzalishaji wa majitaka kwa Manispaa ya Tabora kwa sasa unakadiriwa kufikia lita 15,600,000 kwa siku.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Mtandao wa majitaka katika Manispaa ya Tabora umejengwa sehemu ndogo tu ya mjinikati ambapo ni 8.4% ya wakazi ndiyo wamejiunga na huduma hii.

Asilimia 91.6 wanatumia vyoo vya shimo *(Pit latrine)* pamoja na *septic tanks.* Vyoo hivi vya shimo vimekuwa havikidhi mahitaji ya watumiaji hususani wakati wa mvua.

Maeneo ya Kata zilizopo bondeni za Ng'ambo, Gongoni, Kitete, Tambukareli, Malolo, Isevya, Ipuli pamoja na Cheyo, vyoo vyao vimekuwa vikijaa maji majira yote ya mvua na hivyo kulazimika kunyonya mara kwa mara kwa kutumia magari ya majitaka na kwenda kumwaga kwenye mabwawa yasiyo na ubora yaliyopo Milambo Barracks. Mabwawa hayo yalijengwa ili yatumike kwa muda mfupi na kwa sasa hayana uwezo wa kutibu Majitaka kufikia kiwango kinachoruhusiwa kumwagwa kwenye mazingira au kutumika kwa kilimo kutokana na ongezeko kubwa la uzalishaji wa Majitaka.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Ili kuboresha mazingira ya Manispaa pamoja na Afya za Wananchi, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetoa kibali kwa TUWASA kujenga mabwawa mapya makubwa ya kutibu Majitaka yanayokusanywa kwa njia ya Maboza kutoka kwenye makazi na sehemu za biashara.

Mabwawa haya yatajengwa eneo la Milambo Barracks pembezoni mwa yale ya zamani. Utekelezaji wa mradi huu utagharimu kiasi cha shilingi **Billioni moja, Millioni mia sita ishirini na nane, Mia nane thelathini elfu, mia mbili themanini na tisa na senti sabini na sita tu (1,628,830,289.76). Mradi utatekelezwa na Mkandarasi PERITUS EXIM PRIVATE LIMITED) kutoka Dar Es Salaam.**

Bodi na Menejimenti ya TUWASA inatoa shukurani nyingi kwa **Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan** pamoja na Viongozi wetu Wakuu wa Wizara ya Maji kwa namna

wanavyojali afya za Watanzania wote wakiwemo wakazi wa Manispaa ya Tabora kwa kukubali kutenga fedha hizi kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kutibu Majitaka.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

**Katika kutekeleza mradi huu, kazi zifuatazo zitafanyika:-**

(i) Ujenzi wa mabwawa mawili (2) aina ya *Anaerobic* yatakayotumika kupokelea Majitaka yanayoletwa na Maboza.

(ii) Ujenzi wa Mabwawa mawili aina ya *Facultative* yanayotumika kutibu Majitaka kibailojia.

(iii) Ujenzi wa aridhioevu (*wetland*) kwa ajili ya kusafisha maji zaidi na kuondoa *nutrients.*

(iv) Ujenzi wa chemba mbili (2) za kumwagia magari/maboza.

(v) Ujenzi wa eneo la kukaushia taka ngumu (*Drying beds*).

(vi) Ujenzi wa kijumba kidogo maalum kwa ajili ya kuchomea taka ngumu (Incinerator).

(vii) Ujenzi wa uzio kuzunguka mabwawa.

(viii) Ununuzi wa gari moja (1) la kunyonya majitaka.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Ujenzi wa mradi huu utachukua miezi 12. Hata hivyo, kwa kuwa mradi huu una msamaha wa Kodi ya ongezeko la thamani (VAT), utekelezaji wake umepangwa kuanza mara moja baada ya kupatikana kwa msamaha huo.

Aidha, Mradi huu utakapokamilika, utaboresha usafi wa mazingira na afya kwa wananchi wa Manispaa ya Tabora, Utatoa fursa ya kilimo cha mbogamboga kwa kuwa maji yatakayotoka yatakidhi viwango vinavyotakiwa

kwa kilimo cha umwagiliaji. Pia, Mradi utaongeza ajira hasa katika hatua ya ujenzi na kipindi cha uendeshaji wake.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi - Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Pamoja na mradi huu wa ujenzi wa mabwawa mapya ya kupokea majitaka kwa njia ya magari/Maboza, Manispaa ya Tabora bado ina uhitaji mkubwa wa kupata huduma ya majitaka kwa njia ya mtandao. Kama nilivyosema, takribani asilimia 91.6 ya wakazi wote wa Manispaa ya Tabora wanatumia vyoo vya shimo. Pindi vyoo vinapojaa, Wananchi hulazimika kunyonya mara kwa mara kwa kutumia magari ya majitaka ambapo hulipia kiasi cha shilingi 60,000/- hadi 80,000/ kwa *trip* moja. Hali ya kipato cha wakazi wa Manispaa walio wengi ni ya chini hivyo baadhi yao hushindwa kumudu gharama hizi za mara kwa mara na kuamua kutapishia vyoo vyao kwenye mifereji ya maji nyakati za mvua. Hali hii huwa ni hatarishi kwa mazingira na huchangia kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko.

Kwa kuzingatia hilo, Wizara ya Maji pamoja na TUWASA zimeanza hatua ya awali ya kupata Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa uondoshaji majitaka katika Manispaa ya Tabora. Mradi huo utajumuisha ulazaji wa mabomba ya kukusanya Majitaka kwenye makazi ya watu pamoja na ujenzi wa Mabwawa ya kutibu majitaka kwenye maeneo ya Mansimba (nyuma ya *Airport*) na Kitongoji cha Igange kata ya Malolo. Maeneo hayo tayari yametengwa na Halmashauri ya Manispaa kwa ajili ujenzi wa mabwawa hayo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi – Mkuu wa Mkoa wa Tabora**

Baada ya maelezo hayo, napenda kukushukuru tena na naomba kuwasilisha.

## ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.